



BARAZA LA SANAA LA TAIFA-BASATA

NATIONAL ARTS COUNCIL





# JARIDA LA MSANII

Toleo la nne

Disemba 2023.

# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**
Dkt. Kedmon Mapana

**WAHARIRI**
Lucy Mbogoro
Godfrey Nago

**MWANDISHI**
Isack Bilal

**MSANIFU**
Nicholaus Jofrey

# YALIYOMO

01 Kubwa 3 za BASATA zawekwa hadharani zatikisa tasnia ya Sanaa nchini

02 THT yapewa "maua yao" program ya Kipepeo Mweusi

03 Sanaa kwa Watoto yazalisha Sanaa klabu Meru

04 Elimu ya muziki yawafikia wanafunzi 853 mkoani Arusha

05 Sanaa za Maonesho waomba kuandaliwa Tuzo zao ili kutia hamasa

06 Wasanii waliobeba Tuzo nje ya nchi "wala shavu"

07 Msigwa asisitiza maadili akizindua 3 kubwa za BASATA

08 Mwongozo kuwa chachu ya maadili safi katika maudhui ya Sanaa

09 Waandaaji "Hapa Awards" watia maguu nchini

10 Kamati ya kimkakati kuipaisha TMA kimataifa

11 BASATA Vibes & Sanaa mtaa kwa mtaa yazidi kushika kasi katika mikoa mbali mbali nchini

12 Picha na matukio mbali mbali

# Kubwa 3 za BASATA zawekwa hadharani zatikisa tasnia ya Sanaa nchini

Hatimaye shauku ya wananchi na wapenzi wa Sanaa nchini imemalizwa katika ukumbi wa Peacock Hoteli mara baada ya Katibu mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Bwana Gerson Msigwa kuzindua rasmi Bodi ya Baraza, Mwongozo wa maadili na Kamati ya Tuzo za Muziki Tanzania katika tukio maalum lililofahamika kwa jina la Kubwa 3 za BASATA lililoadhimishwa tarehe 03 Novemba, 2023 na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa Sanaa.

Akiongea wakati wa uzinduzi huo, Katibu mkuu Msigwa amewataka wasanii na wadau wa Sanaa nchini kuwa mstari wa mbele katika kutoa kazi zenye maudhui yanayotangaza vivutio na utamaduni wa Kitanzania ili kuwa sehemu ya kuhamasisha watu kutoka mataifa mbalimbali kutamani kuitembelea nchi ya Tanzania jambo ambalo litasaidia kukuza soko la Sanaa na utalii.

"umefika muda sasa wasanii wetu waanze kufikiria na kufanya kazi za Sanaa kwa ubunifu huku wakitenegenza mahudhui yanayoonesha au kufichua utajiri wa vivutio tulivyo navyo, utamaduni wetu ambao upo tofauti na wengine hii itakuwa chachu kwa watalii na wawekezaji kufanya maamuzi kutembelea nchini kwa minajili ya kuwekeza jambo ambalo litainua soko la Sanaa na utalii" amesisitiza Msigwa juu ya hapo, katibu mkuu ameongeza kuwa, serikali ya awamu ya sita imeamua kwa dhati kuongeza ufanisi katika sekta ya Sanaa hivyo imefanya uteuzi mzuri wa wajumbe wa Bodi wanooongozwa na Mwenyekiti wake Profesa Saaduni….ambaye ana uzoefu mkubwa utakaotumika kusaidia kufikia wadau mbalimbali watakaosaidia kufika malengo tarajiwa.

Serikali haijaishia hapo bali imeenda mbali Zaidi kwa kuweka Mkakati Madhubuti wa kuthamini kazi za wanamuziki kwa kurejesha programu ya tuzo ambayo iliachwa kwa muda mrefu kutokana na sababu zisizo za kawaida, ambapo imeteuliwa kamati ya kimakakati yenye wajumbe wa ndani nan je ya nchi wanaotarajiwa kuzifanya Tuzo za muziki Tanzania kuwa na hadhi ya kimataifa.



# THT yapewa ''maua yao'' program ya Kipepeo Mweusi

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Bwana Gerson Msigwa ameipongeza taasisi ya kukuza vipaji ya ''Tanzania House of Talents'' (THT) pamoja na Msanii wa Bongo Fleva Mwasiti kwa kuandaa programu ya kutoa elimu ya Kwa Wasanii wa kike ya namna ya kutambua thamani yao katika safari ya kupambania ndoto zao za Muziki.

Katibu Mkuu Msigwa ametoa pongezi hizo jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa Programu ya Kipepeo Mweusi tarehe 02 Novemba mwaka huu iliyoandaliwa na Msanii Mwasiti kwa kushirikiana na uongozi wa taasisi hiyo.

Akiendelea kuzungumza katika uzinduzi huo Katibu Mkuu amesisitiza uongozi wa THT kufikiria kusambaza programu hiyo Tanzania nzima kutokana na kuwa na changamoto nyingi wanazopitia wasanii wa kike wakiwa katika harakati za kupambania ndoto zao za kufanikiwa kimuziki hivyo ni vema wakapata elimu hiyo.





"Mwakani ningependa tukio hili lifanyike kwa ukubwa zaidi na tuweze pia kujipima elimu hii ya Kipepeo Mweusi imefikia wadau wangapi nchini, pia natoa wito kwa wadau mbalimbali kujitokeza kuunga mkono programu hii itakayowasaidia watoto wa kike nchini waliyonandoto za kuwa Wasanii wa Muziki" alisema Mhe.Msigwa.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa THT Bi. Kemmy Mutahaba ameishukuru serikali kwa kuwapa ushirikiano na kuahidi kuendelea kuongeza ubufuni katika kutekeleza dhima ya kuisaidia jamii kulingana na sera na miongozo ya serikali kwakuwa Programu hii ya ''Kipepeo Mweusi'' imebeba ujumbe wa ndoto kubwa, uthubutu, utofauti na lengo.

# Sanaa kwa Watoto yazalisha Sanaa klabu Meru

Maazimo ya pamoja ya kuanzisha "Sanaa Klabu" yamefikiwa wakati wa kikao cha majumuisho ya utekelezaji wa progarmu ya Sanaa kwa watoto katika shule nne zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mkoani Arusha.

Maazimio hayo yamefikiwa tarehe 02 Disemba, 2023 ikiwa ni sehemu ya mpango endelevu wa kuinua sanaa na vipaji kwa watoto walio katika mfumo maalumu waweze kupata mafunzo na ujuzi wa fani mbalimbali zitakazowasaidia kutimiza malengo yao huku wakizingatia miongozo ya Maadili kwenye mahudhui watakayozalisha.

Akiongea wakati wa kikao hicho Kaimu Mkurugenzi msaidizi sehemu ya muziki BASATA Bwana Manyaga Oden amesema kuwa ikiwa Klabu hizo zitaanzishwa zitakuwa msaada mkubwa katika kuzalisha wataalamu wa muziki na fani nyingine hivyo




nchi itaweza kuzalisha wasanii ambao ni wasomi wanaoweza kuleta ushindani kwa kipindi kitefu katika soko la sanaa kimataifa.



Kwa upande wa afisa Utamaduni Halmashauri ya Wilaya ya Meru Bi Clementina Mbise ameweka wazi kuwa kwa kipindi kirefu wanafunzi walikuwa wanashiriki kuimba nyimbo mbalimbali ikiwemo za uzalendo katika misingi iliyozoeleka hivyo suala la kuanzisha klabu za sanaa litajenga misingi ya kujifunza mara kwa mara.

Programu ya sanaa kwa watoto inaratibiwa na Baraza la Sanaa la Taifa kwa minajili ya kubaini, kuandaa na kuendeleza vya watoto katika sekta ya Sanaa nchini ili kupanua wigo wa ujuzi kulingana na uhitaji wa maudhui bora ya kazi za Sanaa katika jamii.

# Elimu ya muziki yawafikia wanafunzi 853 mkoani Arusha

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Sehemu Muziki BASATA Bwana Manyaga Oden amefanikiwa kutoa elimu ya ustadi katika uimbaji wa nyimbo za kizalendo kwa wanafunzi 853 katika shule za msingi Leganga, Kilimani, Patandi na Sekondari ya Uraki na Kisimiri Wilayani Arumeru Mkoani Arusha.

Elimu hiyo imetolewa tarehe 02 Disemba, 2023 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa progarmu ya sanaa kwa watoto inayolenga kubaini watoto wenye vipaji ili kuwajengea misingi itakayowakuza katika kufanya shughuli za sanaa katika maadili na kujali uzalendo.

Pamoja na elimu hiyo kila shule imepatiwa nakala moja ya nyimbo ya Taifa na uzalendo kwa mfumo wa sauti na maandishi (mashairi) ili iwe nyenzo za kujifunzia ambapo ufuatiliaji wa mara kwa mara utafanyika.

Aidha, walimu viongozi katika shule hizo na kwa nyakati tofauti wamelishukuuru Baraza kwakuwa hawakuwahi kupata mtaalamu wa kuwaelekeza watoto namna ya kuimba kiustadi nyimbo za uzalendo hivyo kupitia mafunzo hayo na nyenzo walizokabidhiwa itasaidia kuwa na mpango mkakati endelevu wa kiwajenga watoto katika ufanisi wa shughuli za Sanaa.



# Sanaa za Maonesho waomba kuandaliwa Tuzo zao ili kutia hamasa




Raisi wa Shirikisho la Sanaa za Maonesho (SHISAMA) nchini Bi. Cynthia Henjewele ameiomba serikali kuandaa utaratibu utakaofanikisha uwepo wa tuzo za wasanii wanaofanya vizuri katika fani ya maonesho nchini ili iwe chachu kwao kuendelea kufanya vizuri kama inavyotokea kwa Sanaa zingine kama muziki na mitindo.

Ameyasema hayo mbele ya katibu mkuu wakati wa hafla ya Tatu kubwa za BASATA ambapo ameishukuru sana serikali ya awamu ya sita kwa jitohada mbalimbali inazofanya kuhakikisha tasnia ya Sanaa inasonga mbele kwa mafanikio makubwa nchini jambo ambalo linampa mguso wa kuiomba iwafikirie wasanii wa Sanaa za maonesho kwa kuwaanzishia tuzo zitakazowapa morali ya kufanya vizuuri Zaidi.

Henjewewele amebainisha kuwa Sanaa za maonesho inaendelea kukua kwa kasi nchini huku ikitoa mwanga kwa wananchi mbalimbali kufanya kuwa chanzo sahihi cha mapato hivyo ameiomba serikali kuweka nguvu kwaajili ya kulinda ajira zinazopatikana kupitia fani hiyo.
Ameedendelea kusema kuwa kwa muda mrefu sasa vijana na watu wa rika mbalimbali wameweza kujiajiri kupitia Sanaa za maonesho huku akitolea mifano uwepo wa washereheshaji ambao katika jamii ya sasa siyo tu wanaheshimika bali wanajitengenezea vipato halali vinavyosaidia kuinua kada zingine kutokana na ufanyaji kazi unaotegemeana.

Ameongeza kuwa, sasa hivi kuna makund mengi ya sarakasi ambayo yanaiwakilisha viozuri nchi ya Tanzania wakiwemo Ramadhan Brothers ambao kila uchwao wanapata safari katika nchi mbalimbali kushiriki mashindano ya kusaka vipaji vya sarakasi ambako wanafanya vizuri na kuweka alama ya wafuatiliaji kuifahamu nchi, kwahiyo ni muda sashihi kuwahodhi vipaji vya vijana kama hawa kwa kuandaa tuzo au utaratibu wa kuonesha kuthamini kile wanachokifanya.

# Wasanii waliobeba Tuzo nje ya nchi "wala shavu"

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Bwana Gerson Msigwa amewasisitiza wasanii kuzalisha maudhui ya kimkakati yatakayoipa serikali ushawishi wa moja kwa moja kuweza kufanya uwezeshaji wa kazi husika ziweze kufanyika na kufikia malengo tarajiwa.

Ameyasema hayo, leo tarehe 21 Novemba, 2023 wakati wa hafla ya kuwapongeza wasanii walioshinda tuzo mbalimbali nje ya nchi hali inayodhihirisha kukua kwa sekta ya sanaa nje ya mipaka ya Tanzania jambo ambalo linaongeza chachu miongoni mwa wasanii na wadau wa sanaa kuongeza ubunifu utakaofanikisha malengo ya muda mrefu.

Amewahimiza wasanii kuwa mstari wa mbele kutengeneza mahudhui yenye kutangaza rasilimali na vivutio vya Tanzania ili kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato katika sekta ya sanaa.

Katibu Mkuu ameendelea kusema kuwa, kitendo cha wasanii kupata tuzo mbalimbali nje ya Tanzania si la kubezwa bali liangaliwe kwa jicho la upekee ili kuwa mstari wa mbele kutumia jukwaa hilo kutengeneza mahudhui yenye kutangaza rasilimali na vivutio vya Tanzania ili kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato katika sekta ya sanaa.

Kwa kiasi kikubwa serikaki inatambua mchango mkubwa wa wasanii wa Tanzania katika maendeleo ya nchi hivyo umefika wakati sahihi kwao kutoa kazi za kimkakati zinazoonesha uzuri wa vivutio vilivyopo na itakuwa rahisi kuwezeshwa kukiwa na maudhui ya muktadha huo.

Pamoja na sekta kupata wasimamizi wanaobeba maono ya Serikali ya Awamu ya Sita juu ya kufufua, kukuza na kuendeleza Sanaa kimkakati, wasanii wenyewe wanatakiwa kuamka na kuona uelekeo wa serikali yao kuchambua sera ili watoke na sanaa yenye ubunifu kwa minajili ya maendeleo ya Sanaa na jamii kwa ujumla.



# Msigwa asisitiza maadili akizindua 3 kubwa za BASATA

Wizara ya Sanaa Utamaduni na Michezo imesema ina mipango ya kuunda mkakati wa ukuzaji wa sanaa, kwa kuanisha maeneo yenye mafanikio na kuyaangazia, pamoja na kuangalia njia za kuboresha maeneo yenye changamoto.

Hayo yamesemwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo Gerson Msigwa wakati akizindua Tatu Kubwa za Baraza la Sanaa la Taifa (Basata) amesema mkakati huo utajikita katika kukuza shughuli zinazohusiana na sanaa, kuongeza ufikiaji wa sanaa kwa watu wa ndani na nje ya nchi.

Msigwa ameeleza kuwa kwa kuzingatia tasnia inayoongoza kwa ukuaji katika uchumi wa mwaka jana, angependa kuona tasnia hiyo ikidumisha kasi yake ya ukuaji.

“Mafanikio hayo yanaweza kupatikana kwa juhudi za pamoja za viongozi wa serikali, taasisi na wadau."

Katika kubwa tatu, kulikuwa na uzinduzi wa muongozo wa uzingatiaji wa maadili katika kazi ya sanaa ambapo Msigwa amesema miongozo ya maadili inalenga kuwawezesha wasanii kufanya kazi kwa raha na kukumbatia tamaduni za Kitanzania badala ya tamaduni za kigeni.

Katibu Mtendaji wa Basata Dkt. Kedmon Mapana amesema miongozo hiyo inalenga kuwawezesha wasanii na wadau wa sanaa kushiriki moja kwa moja katika kulinda maadili wakati wa kuandaa kazi zao za sanaa.




Pili, inalenga kutatua changamoto za ukiukwaji wa maadili unaotokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika sekta ya sanaa.

Pia ametoa rai kwa wasanii kutengeneza kazi zenye Maadili kwani wao wamebeba maisha ya watu hivyo kubomoa au kujenga itatokana na sanaa huku akimtoa mfano Mwamuziki kutoka Wasafi Nasib Abdul maarufu kama "Diamond platinum " kuwa na wafuasi wengi mtandao wa kijamii ambao wanamfatilia hivyo mtandao huo ukitumika vizuri unaweza kuleta tija kwa jamii.

Mbali na muongozo, kulikuwa na uzinduzi wa Bodi ya Baraza la Sanaa la Taifa na Kamati ya Kitaifa ya Tuzo za Muziki (TMA).

# Mwongozo kuwa chachu ya maadili safi katika maudhui ya Sanaa







Siku za hivi karibuni Kumekuwa na wadau wasio waaminifu ambao kwa makusudi wameanza kutumia Kazi za sanaa katika kuhamasisha na Kupenyeza maudhui yenye ajenda zinazoshawishi nia ovu kinyume na maadili ya jamii na kizazi pendwa cha Watanzania.

Maendeleo ya ukuaji wa teknolojia yamechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa wasanii pamoja na kazi za sanaa zinazosambazwa na kuwafikia kwa urahisi walaji wao kwa njia ya kuwashirikisha kupitia mfumo wa kutengeneza wafuasi kwenye mitandao ya kijamii.

Sheria hiyo inamtaka msanii na mdau wa Sanaa kuhakikisha kazi yake imekidhi matakwa na kupata ithibati ya Baraza iwapo itakuwa imezingatia mambo ya kimaadili yafuatayo;

Haivunji heshima na utu wa mtu yeyote;

- Haina upotoshaji wa aina yoyote;
- Haichochei ghasia ya aina au namna yoyote;
- Haina maneno ya uongo, uchochezi au yanayokashifu watu wengine;
- Haihudhurishi lugha chafu au matusi;
- Haina ujumbe wa unyanyasaji au ukatili;
- Haitukuzi ubaguzi wa rangi, jinsi, kabila au dini;
- Haikashifu Taifa la Tanzania au mataifa mengine;
- Haidhoofishi umoja, ushirikiano na ustawi wa jamii;
- Haishawishi vitendo vya kihalifu, au uvunjifu wa sheria za Tanzania, za kimataifa, au za mataifa mengine;
- Haishawishi wala kuhamasisha vitendo vya ngono, ushoga, usagaji, ulawiti na matumizi ya dawa za kulevya;
- Inazingatia masharti ya sheria za Tanzania na mikataba mbalimbali ya kimataifa katika masuala ya hakimiliki na masuala mengine yote yanayohusiana na haki za ubunifu

Hivyo basi Baraza la Sanaa la Taifa linawasisitiza wasanii na wadau wa fani zote za Sanaa wakiwemo wasanii wa Muziki, Watayarishaji wa maonesho ya mavazi na mitindo, wapambaji, waongozaji wa Video za muziki na wamiliki wa kumbi za starehe na sanaa nyinginezo kutumia mwongozo huo ili kutoa kazi zenye kuzingatia maadili ya Kitanzania.

# Waandaaji ''Hapa Awards'' watia maguu nchini

Wakiwa hapa nchini Waandaaji hao wamefanikiwa kukutana na kufanya vikao na Viongozi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo lengo likiwa kujadiliana namna ya kuwa na mkakati wa Pamoja kuendeleza sekta ya Sanaa nchini iweze kuwa na mtazamo wa kibaishara.

Pamoja na majadiliano hayo, waratibu wa ''Hapa Awards'' wakiambatana na Katibu Mtendaji BASATA Dkt. Kedmon Mapana wamefanikiwa kutembelea katika Taasisi ya Sanaa Bagamoyo-TaSuBa ambako waliweza kujionea urithi wa Sanaa unavyoweza kuenezwa miongoni mwa jamii ya Kitanzania kupitia mafunzo yanayotolewa pia waliweza kuahidi kushiriki katika uandaaji wa tamasha la Kimataifa la Utamaduni Bagamoyo la mwaka 2024.

Wakiongea kwa nyakati tofauti, Bi. Amber Washington na Tina Weisinger wamekiri kufurahishwa na jitihada zinazofanywa na serikali katika kukuza na kuendeleza sekta ya Sanaa nchini jambo ambalo hata wao limewavutia na kushawishika kuwa ipo siku Tuzo za ''Hapa Awards'' zitafanyika katika nchi ya Tanzania ili kusaidia kuleta wadau kutoka mataifa mbalimbali Duniani katika dhana ya kuimarisha ushirikiano







Tuzo za ''Hapa Awards'' zinaandaliwa na kuratibiwa na Bi. Amber Washington ambaye pia ni Mwanzilishi na Mtendaji Mkuu Hollwood nchini Marekani ambazo zimejikita kutambua michango ya heshima kwa wadau na wasanii mbalimbali katika kuendeleza sekta hiyo Marekani na nchi za Afrika hususani namna ya kufanikisha sekta ya Sanaa kuwa biashara inayoweza kuwa chanzo thabiti cha mapato.



# Kamati ya kimkakati kuipaisha TMA kimataifa




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Damas Ndumbaro ameteua kamati ya kimakakati inayojumuisha wajumbe wenye weledi na uzoefu wa kutosha kuendesha masuala ya muziki ndani na nje ya nchi ili waweze kuratibu na kuendesha Tuzo za muziki Tanzania (TMA) kwa lengo la kuzifikisha katika hadhi ya kimataifa.

Ikumbukwe kuwa moja ya programu inayoratibiwa na Baraza la sanaa la Taifa ni utoaji wa ya Tuzo za Muziki ambayo ilisimama kwa miaka zaidi ya nane kabla ya kurejeshwa tena mwaka 2021 ikisimamiwa na Serikali kwa asilimia 100 ikihusisha utoaji wa zawadi kwa wanamuziki waliofanya vizuri katika kipindi maalum cha mwaka husika.

Aidha, programu hii imejikita katika utoaji wa Tuzo kwa wanamuzi wa Tanzania kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji wa kazi bora za muziki zilizojaa ubunifu bila ya kuathiri mila na desturi.
Sambamba na utoaji wa tuzo kwa wanamuziki mahiri nchini, pia zinahusisha wanamuziki wa nchi nyingine toka Mashariki, Kusini na Magharibi mwa Afrika ikiwa ni sehemu ya kutambua ushirikiano wa kazi za sanaa Kimataifa.

Baraza la Sanaa la Taifa linasimamia uratibu stahiki wa Tuzo za Muziki kwa nia ya kufufua, kukuza na kuendeleza Tasnia ya Muziki na Wanamuziki nchini Tanzania, dhumuni kubwa la kuifungua programu ya Tuzo za Muziki ni kuifanya ifikie hadhi ya kimataifa ndiyo maana serikali kupitia Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo akateua wajumbe wa kamati kimkakati kama ifuatavyo;

- David Minja (Mwenyekiti):

Mtaalamu wa kimataifa wa masoko na biashara.
Amewahi kuwa mkurugenzi mkuu wa kampuni ya Unilever Tanzania, Mkurugenzi wa masoko TBL ambapo alihusika kwa kiwango kikubwa kuijenga Kilimanjaro Tanzania Music Awards na kuanzisha kwa Kili Music Awards Tour.

- Christine Mosha "Seven" (Makamu Mwenyekiti):

Mkuu wa Muziki na Maendeleo ya Wanamuziki Afrika Mashariki wa Kampuni ya Sony Music Entertainment; Alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Rockstar Africa; na Mkuu wa Biashara wa Kituo cha MTV Base Africa (East Africa). Amewahi pia kuwa mtangazaji wa East Africa Radio na TV, na Redio ya Clouds FM.

- Mrisho M. Mrisho (Katibu):

Ofisa mwandamizi katika Baraza la Sanaa la Taifa BASATA) na ana uzoefu katika masuala ya masoko, fedha na biashara. Pia, ni mwanzilishi wa wazo la kurejesha TMA 2021, na alikuwa mratibu wa TMA 2021 na 2022.

- Paul Matthysse "Pfunk" (Mjumbe):

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bongo Records na ana uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika shughuli za sanaa na muziki hapa nchini.

- Chris Torline (Mjumbe):

Raia wa Afrika Kusini na ni kiungo muhimu kati ya TMA na wadau wa kimataifa. Mkurugenzi Mkuu wa Ukuzaji wa Masoko na Kampeni, mwenye uzoefu kwenye Udhamini. Kwa miaka 23, Chris ametumikia wa mafanikio nyadhifa zinazoheshimika kwenye Uzalishaji wa Maudhui, zaidi yahapo, amefanikiwa katika kuandaa na kuratibu matukio makubwa kama vile Tuzo za Muziki za MTV Afrika nchini Nigeria, Kenya, na Afrika Kusini, Nickelodeon Nickfest nchini Afrika Kusini na Nigeria, BET Experience Africa, na Tamasha la Vichekesho la Kimataifa la Afrika.

- Natasha Stambuli (Mjumbe):

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Transs Net (Boomplay) inayosimamia uuzaji wa kazi za muziki kidigitali. Mwanachama wa Akademia ya Tuzo za Grammy, Makamu Mwenyekiti wa Women in Music taasisi yenye makao makuu New York nchini Marekani, zaidi ya hapo ni mwanzilishi wa Igloo Entertainment ambayo ni Kampuni ya kukuza vipaji nchini.

# BASATA Vibes & Sanaa mtaa kwa mtaa yazidi kushika kasi katika mikoa mbali mbali nchini



BASATA Vibes ni mradi wa Sanaa iliobuniwa na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kwa kushirikiana na Kituo cha Utamaduni cha Ufaransa kilichopo jijini Dar Es Salaam na kinachotambulika kwa jina la Alliance Francaise Kwa kufanya mambo makuu mitatu kama ifuatavyo.

i. Kufanya mafunzo ya maafisa Utamaduni na wadau wa Sanaa juu ya uandaaji Bora wa matukio nchini

ii. Kutuma ujumbe wa Tanzania Nchini Ufaransa kuhudhuria jukwaa la sanaa na ubunifu wa Kiikolojia baina ya nchi za Afrika na Ufaransa (Euro Africa-Bienalle)

iii. Kuandaa matukio 12 ya sanaa na Burudani kwenye Mikoa Nane, Tanzania Bara na Visiwani. Matukio haya yatakwenda kwa jina la "BASATA VIBES"

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) Kwa kushirikiana na Kituo cha Utamaduni cha Ufaransa (Alliance Francaise ) tumefanikiwa kuratibu matukio manne Kati ya 12 kwenye Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Arusha, na Dodoma na tunatarajia kufikia mikoa yote Tanzania



Programu ya Sanaa Mtaa kwa Mtaa imeanzishwa na Baraza kwa kuzingatia maelekezo ya aliyekuwa Waziri wa Utamaduni,Sanaa na Michezo Mh. Mohamed Omary Mchengerwa (MB) . Kulingana na tukio hili, Sanaa za Ufundi, Maonesho na Muziki zitahusika kwa nia ya kukuza na kuendeleza Sanaa nchini.



Baraza la Sanaa la Taifa, Pamoja na kuanzisha na kuratibu tukio la Sanaa Mtaa kwa Mtaa; tukio hili litakuwa endelevu katika Halmashauri zilizopo nchini ya kwa usimamizi wa Afisa Utamaduni

1.1 Malengo ya Sanaa Mtaa kwa Mtaa

a. Lengo Kuu

Kuibua, Kukuza na kuendeleza Sanaa nchini

b. Malengo Mahsusi

i. Kuwezesha wasanii wa Sanaa mbalimbali kuonyesha kazi zao za Sanaa

ii. Kukata kiu ya jamii ya kuwa na matukio ya Sanaa mitaani

iii. Kuibua na kuendeleza vipaji vya wasanii chipukizi katika tasnia zote za Sanaa




UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
LA SANAA LA TAIFA - BASATA
YA BASATA







